

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA

24 MEI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA – TAREHE 24 MEI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

307. MHESHIMIWA OMAR ABDALLAH KIGODA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):

Je, ni kwa kiasi gani Serikali inasimamia suala la asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri kwa ajili ya Vijana na Kina mama.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

308. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Tatizo la uvuvi haramu bado linaendelea licha ya jitihada za Serikali kuchoma nyavu za uvuvi zisizopendekezwa:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukomesha uvuvi haramu zaidi ya kuchukua hatua hiyo ya kuchoma nyavu.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

309. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Tatizo la Maji katika Jimbo la Wanging'ombe limekuwa sugu kwa sasa:-

Je, ni lini Serikali itatatia tatizo hilo.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

310. MHESHIMIWA DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF (MGOGONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Serikali ilianzisha Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa mujibu wa Ibara ya 133 ya Katiba kupitia Sheria Namba 15 ya Mwaka 1984 ili kila upande usimamie uchumi wake na uchumi wa Muungano usimamiwe na chombo cha Muungano:-

- (a) Je, ni kwa nini kwa miaka 33 sasa Akaunti hiyo haijafanya kazi yake;
- (b) Je, gharama kiasi gani imetumika kuanzisha taasisi ambayo haina faida yoyote.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

311. MHESHIMIWA EMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na ajali nyingi zinazotokana na vitendo vya baadhi ya Askari Polisi maarufu kama PT kuwakamata waendesha bodaboda wakiwa kwenye mwendo huku wakiwa wamebeba abiria. Hali hiyo hupelekea waendesha bodaboda na abiria kupata ajali mara kwa mara:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kuwa ajali za kizembe zinazosababishwa na baadhi ya Askari Polisi zinakomeshwa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**DODOMA
24 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**